

## Maswali

1. Hana aliomba nini?
2. Hana aliahidi Mungu nini?
3. Mtoto wa Hana aliitwa nani?
4. Hana alipeleka Samweli wapi?
5. Kila mwaka Hana alimpa Samweli nini?
6. Nani alikuwa kuhani katika Hekalu?
7. Wana wa Eli walikuwa namna gani?
8. Nani alimuita Samweli usiku?
9. Mungu alimwambia Samweli nini?
10. Eli na wanawe walikufaje?

## Majibu

1. Hana aliomba mtoto.
2. Hana aliahidi Mungu kwamba atampa huyo mtoto.
3. Mtoto wa Hana aliitwa Samweli.
4. Hana alipeleka Samweli Hekaluni.
5. Kila mwaka Hana alimpa Samweli koti ndogo.
6. Kuhani alikuwa Eli.
7. Watoto wa Eli walikuwa wabaya.
8. Mungu alimuita Samweli usiku.
9. Mungu alisema atawaadhibu Eli na watoto wake.
10. Watoto wa Eli walikufa kwa vita na Eli alivunjika shingo.

## SHULE YA JUMAPILI YA CBM



Awamu ya 1 Mwaka wa 1

## 23 Samweli

### Marejeo

1 Samweli 1—3

### Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Mungu husikia maombi yetu na ni lazima tufunze watoto wetu kuomba

### Maneno maalum

1. Elkana + Hana + hana (bila) mtoto + omba mtoto mvulana + ahadi + pea Mungu + Samweli azaliwa + Tembelea hekalu + koti (vazi) ndogo
2. Eli + wana wabaya
3. Sauti inaita + uliza Eli + Samweli ajibu + adhibu Eli
4. Wafilisti wapigana na Israeli + wana wawili wauawa + Eli anaanguka + Eli anakufa

**23.1** Elkana na Hana hawakuwa na watoto. Hana alikuwa na huzuni. Aliomba, "Ee Mungu, ukinipa mtoto, ninaahidi kwamba nitakupa huyo mtoto akutumikie maisha yake yote." Mungu alisikia maombi ya Hana na akapata mtoto aitwae Samweli. Samweli alipokuwa na umri wa kuachwa, Hana alimpeleka hekaluni na kumkabidhi Eli kuhani.


Kila mwaka Hana alienda hekaluni na Elkana. Alienda kumuona Samweli na kumpa koti ndogo alilokuwa ameshona.



**23.2** Eli alikuwa na wana wawili, Hofni na Finehasi lakini walikuwa wabaya na hawakumpenda Mungu. Eli alijua walikuwa wabaya lakini hakuwaadhibu.

**23.3** Wakati moja Samweli alienda kulala, baadaye akasikia sauti ikimwita, "Samweli! Samweli!" Samweli aliruka kutoka kitandani na kukimbia kwa Eli. "Mimi hapa," akasema. "Rudi ulale Samweli sikukuita," Eli alisema.

Samweli alirudi kulala na hiyo sauti ikamwita tena. "Samweli! Samweli!" Samweli mara tena akamkimbilia Eli. Eli alimwambia hakumwita.



Mara ya tatu sauti iliita tena. "Samweli! Samweli!" Samweli alikimbia kwa Eli tena. Eli akatambua ni Mungu alikuwa akimwita Samweli. Eli alimwambia Samweli, "Enda ulale na akikuita tena, lazima useme mtumishi wako amesikia."

Mungu alimwita tena Samweli na akasema vile Eli alimwambia. Mungu akamwambia kwamba ataadhibu Eli na wanawe kwa sababu hawajawambia waniheshimu.

**23.4** Siku moja Wafilisti walikuja kupigana na Waisraeli, wana wawili wa Eli walienda vitani. Waliuawa siku hiyo. Mtu mmoja akakimbia kumwambia Eli. Eli alikuwa amekaa kitini akisubiri habari ya vita.

Alikuwa mzee sana wa miaka tisini na nane. Yule mtu alipokuwa anamkuja akikimbia kuleta habari, Eli aliogopa. "Kumetokea nini?" Eli alimuuliza. "Waisraeli wameshindwa na hata wanao wawili wamekufa."

Eli aliposikia hiyo habari, aliangukia nyuma ya kiti shingo ikavunjika na akafa. Eli alikufa siku moja na wanawe, kwa sababu hakuwa amewafundisha kupenda na kuheshimu Mungu.